Posta
Let's Go!

# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

# JARIDA LA POSTA

JULAI - DISEMBA 2021
ISSUE NO. 001







Posta e-SHOP Let's Go! | EMS | Posta Kiganjani | pCUM CITY URGENT MAIL | posta_tz

# BODI YA WAHARIRI

MWEYEKITI
Macrice D. Mbodo
Kaimu Postamasta Mkuu Shirika la Posta Tanzania

MRATIBU NA MHARIRI WA JARIDA
Elia P. K. Madulesi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Shirika la Posta Tanzania

MWANDAAJI WA JARIDA
Loema Joseph

WAHARIRI
Mashala Lufunga
Jane Sallu
Rachel Kitinya

MSANIFU
Barnabas Raphael

# POSTA ONLINE SHOP




**Unaweza kununua bidhaa mtandaoni kupitia**

**wwww.postashoptz.post**

**Phone: +255 718 900 700**

# POSTAMASTA WAKUU



**Suleiman Msofe**
**Postamasta Mkuu**
**1994-2001**



**Lucian Minde**
**Postamasta Mkuu**
**2001-2007**



**Deos K. Mndeme**
**Postamasta Mkuu**
**2008-2015**



**Fortunatus Kapinga**
**Postamasta Mkuu**
**2015-2017**



**Deogratius C. Kwiyukwa**
**Kaimu Postamasta Mkuu**
**Machi 2017-Novemba 2017**



**Hassan Mwang'ombe**
**Postamasta Mkuu**
**2017-2021**



**Macrice D. Mbodo**
**Kaimu Postamasta Mkuu**
**2021-Sasa**

# YALIYOMO


Makamu wa Rais ashiriki Maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani........1

Shirika la Posta kuchangia uchumi wa buluu Zanzibar........3

Wafanyakazi wa Posta watakiwa kubadilisha mtazamo........10

Ziara ya Kaimu Postamasta Mkuu viwanja vya sabasaba........11

Posta yashiriki Kongamano la ununuzi na ugavi........15

Pongezi uteuzi........16

Waziri Mkuu azindua vituo vya Huduma Pamoja........17

Uzinduzi Duka Mtandao Posta........20

Posta yaingia makubaliano ya kibiashara na Benki ya CRDB ........22

Posta kushirikiana na Shirika la Bima Zanzibar........24

Posta yaingia makubaliano ya kibiashara na TANTRADE........25

Picha za magari yetu ya mizigo ........26

Posta yashiriki mkutano wa Umoja wa Posta Duniani - Ivory Coast ........27

Tanzania yangara kimataifa........28

Ufunguzi wa kikao cha Baraza la Majadiliano la Shirika la Posta........29

Kufungwa kwa kikao cha Baraza la Majadiliano la Shirika la Posta........32

Posta yatoa wasilisho kwa Baraza na Makatibu Wakuu Zanzibar........33

Posta yakutana na Jukwaa la Wahariri Tanzania........35

Ufunguzi wa kikao kazi cha viongozi wa Shirika la Posta ........36

Kufunga kikao kazi cha viongozi wa Shirika la Posta ........37

Ziara ya Postamasta wa Ivory Coast kutembelea Shirika la Posta Tanzania........38

Huduma Pamoja........39

Posta yapokea ugeni kutoka Burundi........40

Katibu mkuu akutana na ugeni kutoka Posta Burundi........53

Dkt Chaula apokea ugeni kutoka Posta wa Kenya........54

Washirika wetu........56

Biashara zetu........57

# MAKAMU WA RAIS DKT. MPANGO AHITIMISHA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amesema Serikali inafurahi uwepo wa uhusiano mkubwa kati ya malengo makuu ya Umoja wa Posta Duniani na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na yale ya Sera ya Taifa ya Posta ya 2003 hasa katika kuwahudumia wananchi.

Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mpango ametoa kauli hiyo wakati akihitimisha siku ya Posta duniani katika maadhimisho ya siku hiyo yaliyofanyika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Akiwahutubia mamia ya wakazi wa mkoa wa Dodoma, wageni kutoka sehemu mbalimbali na watoa huduma washiriki wa huduma za mawasiliano nchini, Dkt. Mpango amesema Serikali imeshuhudia mageuzi makubwa ndani ya Shirika la Posta, kutokana na huduma mbalimbali zilizoanzishwa na Shirika hilo zikiakisi matumizi ya teknolojia katika kuwahudumia watanzania.

"Tumeshuhudia Posta ikibadilisha namna ya utoaji huduma zake kwa jamii kulingana na mahitaji na ndio maana leo hii tunashudia hatua ya Posta kuwa ya kidigitali na kuweza kuwafikia watu wengi kwa urahisi zaidi". alisema Makamu wa Rais Dkt. Mpango.

Mbali na kupongeza jitihada hizo Makamu wa Rais Dkt. Mpango amesema, kupitia Shirika la Posta Tanzania, Serikali inahitaji kuona utendaji wenye tija ikiwa ni pamoja na kuwahudumia wananchi kwa ufanisi kupitia mtandao mpana wa Shirika hilo lenye matawi zaidi ya 350 yaliyosambaa nchi nzima.

Alisema "Ni muhimu taasisi hii iguse jamii kihuduma kwakuwa ilianzishwa ili kuhakikisha inatoa huduma kwa niaba ya Serikali na kuwahudumia wananchi wote bila kujali mahali walipo.

Kwa upande wake Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amesema Wizara yake imefanya maadhimisho hayo kwa siku nne mfululizo na kushirikisha wadau mbalimbali katika Sekta ya Posta na nje ya Sekta ya Posta, nia ikiwa ni kuonesha Umma umuhimu wa huduma za Posta nchini.

Awali akizungumza katika kilele cha maadhimisho hayo Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Rahma Kassim Ali amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa hongera kwa umoja wa Posta duniani kwa kufikisha miaka 147 tangu kuanzishwa kwake akisema siku ya Posta duniani inabeba dhana muhimu sana ya muungano.



# MAKAMU WA RAIS DKT. MPANGO AHITIMISHA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI

"Hata kama hatuongei lugha moja lakini dunia nzima inaunganishwa na nguvu ya barua na mizigo inayowekwa stempu" alisema, Mhe. Rahma Kassim Ali.

Katibu Mkuu Mtendaji wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU), Ndg. Sifundo Chief Moyo ambaye pia ameshiriki katika kilele cha maadhimisho hayo amesema PAPU itaendelea kushirikiana na nchi mwanachama wa umoja huo katika kusambaza taarifa na miongozo pamoja na kufanya tafiti mbalimbali, akisisitiza kuwa dunia haina budi kujifunza kutokana na Janga la UVIKO-19 na majanga mengine kubadilika kulingana na mazingira ili kuweza kuendelea kumudu utoaji huduma kwa wateja .

Posta
Let's Go!

Kila Ifikapo Oktoba 9 ya kila mwaka, Tanzania kama mwanachama wa Umoja wa Posta duniani aliyejiunga mwaka 1963, huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku ya umoja huo ulianzishwa mwaka 1874.



# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo ameeleza namna ambavyo Shirika hilo limejipanga katika kuhakikisha linakuwa moja ya taasisi za Serikali itakayochangia kukuza maendeleo na uchumi Visiwani Zanzibar.

Aliyasema hayo tarehe 23 Novemba, 2021 wakati akizungumza na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Rahma Kassim Ali, katika ofisi za Wizara hiyo Kisauni, Zanzibar

Bw.Mbodo alieleza kuwa, Shirika la Posta nchini linatambua mchango wa Wizara hiyo katika kutengeneza mazingira rafiki hususan kwa wananchi wa Zanzibar katika kutumia huduma za Posta nchini, hasa katika matumizi ya Duka Mtandao lililoanzishwa na Shirika la Posta Tanzania.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara yake ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa upande wake imeendelea kuhamasisha wajasiriamali wadogowadogo na wakubwa visiwani humo kujisajili kwenye Duka hilo kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa bidhaa za Zanzibar duniani kote kupitia Duka hilo

"Posta tunajivunia uwepo wa Wizara hii na jitihada kubwa ambazo zimefanywa na Wizara hii katika kutengeneza mazingira rafiki ya Shirika la Posta kuwahudumia wananchi ikiwemo kuwasajili wajasiriamali wa Zanzibar kwenye Duka Mtandao la Posta ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa za Zanzibar duniani". Alisema Bw. Mbodo.

Itakumbukwa wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani tarehe 9 Octoba, 2021 Shirika la Posta Tanzania liliandaa shindano kwa mjasiriamali atakayeonekana kuuza bidhaa nyingi zaidi nje ya nchi kupitia Duka Mtandao la Posta, ambapo mshindi alikuwa ni Zanzibar State Trade Cooperation (ZSTC) kutoka Zanzibar na alikabidhiwa zawadi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philip Isdor Mpango, jijini Dodoma.

"Takwimu za Mauzo ya duka mtandao zinaonesha kuwa Zanzibar imeuza bidhaa mbalimbali nje ya nchi hususani viungo na hilo linaonesha kuwa bidhaa kutoka Zanzibar zinahitajika duniani," Aliongeza Bw. Mbodo.

Katika hatua nyingine, Bw. Mbodo alifafanua kuwa, Shirika la Posta limejipanga kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kutangaza vivutio vya Utalii kwa kutumia stempu zinazotengenezwa na Shirika hilo lengo ikiwa ni kukuza sekta ya utaliii Visiwani Zanzibar.

Aidha, Stempu hizo zenye vivutio mbalimbali ikiwemo Majengo ya kihistoria ya Zanzibar, Maraisi waliomaliza muda wao visiwani humo zinaweza kupata fursa ya kuuzwa na kupatikana sehemu zote duniani kupitia wakusanyaji wa stempu hizo zaidi ya 60 walioko zanzibar ikiwa ni sehemu ya kukuza sekta ya utalii nchini.

Bw. Mbodo ameongeza kuwa, Shirika la Posta nchini kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Utalii ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar litatambulisha na kutangaza zaidi aina mbalimbali ya vivutio vinavyopatikana Zanzibar na kuziweka katika Stempu sambamba na duka Mtandao ili kuvutia watalii wengi zaidi duniani.

Vilevile Shirika la Posta Tanzania limejipanga kuhakikisha linakuwa miongoni mwa taasisi zitakazochangia maendeleo ya ukuaji wa uchumi Visiwani Zanzibar kwa kuendelea kutoa huduma bora na stahiki zenye tija kwa wanachi wa Zanzibar kulingana na mahitaji ya soko.

"Tunaiomba Serikali ya Mapinduzi zanzibar kuendelea kutoa ushirikiano kwa Shirika la Posta ili liweze kuwa miongoni mwa taasisi ambazo zinaweza kuchangia maendeleo ya uchumi wa buluu Zanzibar". Alisema Bw. Mbodo

Posta
Let's Go!

# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

Wakati huo huo, Kaimu Postamasta Mkuu ameelezea mashirikiano yaliyopo baina ya Shirika la Posta Tanzania na Taasisi mbalimbali zilizopo visiwani Zanzibar ikiwemo Shirika la Bima Zanzibara (ZIC), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wa pande zote mbili za Muungano wanapata huduma stahiki na kwa wakati.

"Shirika la Posta ni Taasisi ya Muungano na tuna ofisi zaidi ya 350 kote nchini, kwa hiyo tunauwezo kufikishiwa huduma kwa wananchi kokote walipo nchini". Amesema Mbodo.

Katika hatua nyingine, Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta alipata nafasi adhimu ya kukabidhi Zawadi ya saa maalumu kwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (Zanzibar) Mhe. Rahma Kassim Ali pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Amour Hamil Bakar zenye Nembo ya Shirika la Posta, picha za stempu zenye vivutio vilivyopo Zanzibar, picha ya magari kuonesha huduma ya usafirishaji, na duka mtandao la Shirika ikiwa ni sehemu ya huduma za Shirika la Posta zenye lengo la kukuza maendeleo ya uchumi wa buluu Zanzibar.

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali amelipongeza Shirika la Posta Tanzania kwa kazi kubwa na maboresho makubwa yanayofanywa na Shirika hilo katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora Zanzibar na nchini kote.

"



Niwapongeze kwa shughuli ambazo mnazifanya ikiwemo kuitangaza Zanzibar kiutalii, hiyo itapelekea kuvutia watalii wengi zaidi hatimaye kukua kwa uchumi Zanzibar. Alisema Mhe. Rahma".

Aidha, Mhe Waziri amelitaka Shirika la Posta nchini kuendelea kuwekeza katika kujitangaza zaidi hasa kwa upande wa Zanzibar ili wananchi waendelee kuvutiwa zaidi na uboreshwaji wa huduma mbalimnali zilizofanywa na Shirika la Posta nchini

"Hili ni Shirika la wananchi wanapaswa kulijua kwa sababau na wao watatumia fursa hizo katika shughuli zao mbalimbali". Alisema Mhe. Rahma.

Mhe. Waziri ameahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Shirika la Posta nchini ili kuhakikisha wananchi wa pande zote za Muungano wanapata huduma bora na zenye tija kwa manufaa ya Taifa.

# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo akizungumza wakati wa kikao na Menejimenti ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kulia ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Zanzibar Ndg. Amour Hamil Bakar akizungumza wakati wa kikao kati ya wizara tajwa na Shirika la Posta nchini, Kushoto ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali.

# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali akizungumza wakati wa kikao na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania katika ofisi za Wizara hiyo Kisauni, Zanzibar.



Viongozi waandamizi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wakifuatilia kikao kati ya Wizara hiyo na shirika la Posta nchini, katika ofisi za wizara hiyo Kisauni, Zanzibar

# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR



Baadhi ya viongozi wa Shirika la Posta Tanzania wakifuatilia mkutano baina ya Shirika hilo na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika ofisi za Wizara hiyo Kisauni, Zanzibar. Kulia ni Meneja Mkaazi Zanzibar Bw. Ahmad Mohamed Rashid.




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo akiielezea picha na vivutio mbalimbali vinavyoonekana kwenye saa aliyoitoa kama zawadi kwa waziri wa Ujenzi. Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali (wapili kulia) pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Amour Hamil Bakar (kulia), mara baada yamkutano wao.

# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo (kushoto) akikabidhi saa maalum kama zawadi kwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Rahma Kassim Ali (kulia).




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo (kushoto) akikabidhi saa maalum kama zawadi kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Ndg. Amour Hamil Bakar (kulia).

# SHIRIKA LA POSTA KUCHANGIA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR



**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Rahma Kassim Ali (katikati aliyekaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi waandamizi kutoka Shirika la Posta Tanzania , mara baada ya mkutano nao katika ofisi za Wizara hiyo Kisauni Zanizbar. Kushoto (aliyekaa) ni katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Amour Hamil na kulia ni Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta nchini Bw. Macrice Daniel Mbodo**




**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (Zanzibar) Mhe. Rahma Kassim Ali (katikati) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndg. Amour Hamil Bakar (kushoto) katika picha ya pamoja wakiwa wameshika zawadi zao walizokabidhiwa na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta nchini Bw. Macrice Daniel Mbodo (kulia), mara baada ya mkutano wao, katika ofisi za Wizara hiyo kisauni Zanizbar**

# WAFANYAKAZI SHIRIKA LA POSTA WATAKIWA KUBADILISHA MTAZAMO

SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC) limewataka wafanyakazi wake kubadilisha mtazamo wao na kuendana na mfumo wa kidijitali.

Hayo yamesemwa na Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara za Shirika la Posta Tanzania Bw. Constantine Kasese alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Posta Mkoa wa Morogoro katika ofisi za Posta Mkoani humo mara baada ya kuhitimisha kikao cha siku mbili cha Baraza la Majadiliano la Shirika hilo kilichofanyika mkoani humo.

Bw. Kasese alitarabaisha kuwa Serikali imewekeza fedha nyingi ndani ya Shirika hili ili kuboresha mfumo wa kidigitali na hilo linaenda kuongeza mapato

Wafanyakazi wanatakiwa kufanyakazi kwa ubora kila mmoja kwenye eneo lake ili kuongeza tija na mapato ndani ya Shirika na kuchangia mapato ya Serikali

Ameeleza kuwa, mameneja wa mikoa watumie rasilimali zilizopo kuwafikia wananchi na kuwapatia elimu ya huduma zinazopatikana ndani ya Shirika hilo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa wateja.

"Kuna huduma zimerahisishwa ikiwemo Huduma mpya ya "Virtual Box" ambayo namba yako ya simu ndiyo sanduku lako la Posta, Posta Kigangani na kuna huduma zingine zinakuja na zote zitapatikana ndani ya Shirika la Posta, hivyo hakilisheni mnakuwa mabalozi wazuri wa huduma zetu". Alisema Kasese.

Bw. Kasese alitumia wasaa huo pia kuwajulisha wafanyakazi wa Shirika Mkoa wa Morogoro juu ya maadhimisho ya wiki ya Posta ambayo kilele chake kitakuwa tarehe 9 oktoba

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Philip Mpango.

Kwa upande wake Kaimu Meneja Mkuu Rasilimali za Shirika la Posta Aron Samwel amewataka wafanyakazi wa Shirika hilo mkoani Morogoro kuwajibika na kujituma katika nafasi zao, kufikia malengo waliyowekewa na Shirika katika utendaji na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kuongeza mapato ya Shirika

"Hakikisheni mnajituma na kuyafikia malengo mliyowekewa katika nafasi zenu na myatekeleze kikamilifu malengo mliyopatiwa". Alisema Aron

Sambamba na hilo, Aron aliwasisitiza wafanyanyakazi hao kuwa na ukarimu na kujali wateja (Customer Care) pindi wafikapo kupata huduma katika ofisi za Posta ili kuendelea kuwafanya wateja kufurahia huduma za Posta.







Posta
Let's Go!

# ZIARA YA KAIMU POSTAMASTA MKUU KATIKA VIWANJA VYA SABASABA

Kaimu Postamasta Mkuu Macrice Daniel Mbodo ametembelea banda la Shirika la Posta kwenye maonesho ya sabasaba yanayoendelea. Katika ziara yake ya kutembelea banda la Shirika la Posta viwanja vya maonyesho ya Sabasaba, jijini Dar es-salaam, alikutana na Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka ya maendeleo ya biashara Tanzania(TanTrade) Mhe. Balozi Mteule Edwin Rutageruka

Aidha, akiwa ziarani hapo Kaimu Postamasta mkuu alipata nafasi ya kuonana na Bilionea wa madini ya Tanzanite Bwana Saniniu Laizer ambaye pia alikuwa viwanjani hapo.
Bwana Saniniu alitembele banda la Shirika la Posta lililopo katika viwanja vya Sabasaba na kujionea fursa mbalimbali za kibiashara zinazopatikana Posta



*Kaimu Postamasta Mkuu Macrice Mbodo (kushoto) akiwa katika Picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade Mhe.Balozi Mteule Edwin Rutageruka (wa nne kulia) Pamoja na Billionea wa madini Saniniu Laizer (wa tatu kushoto) Katika ofisi za mkurugenzi wa TanTrade, Dar es Salaam*

*Billionea wa madini Saniniu Laizer (Aliye kaa kushoto) Alipotembelea banda la Shirika la Posta. Kulia aliyekaa ni Postamasta Mkuu wa shirika hilo Macrice Mbodo*



# ZIARA YA KAIMU POSTAMASTA MKUU KATIKA VIWANJA VYA SABASABA

Wakati wa ziara hiyo Kaimu Postamasta mkuu Macrice Daniel Mbodo alipata nafasi ya kuonana na Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) Bi. Justina Mashiba ambaye pia alitembelea banda la Posta kujionea mabadiliko Mbalimbali yaliyofanywa na Shirika katika utoajiwa huduma zake.

Bi. Justina mashiba amefurahishwa na uboreshwaji wa huduma za Posta na alimpongeza kaimu Postamasta Mkuu Bwana Mbodo kwa namna ambavyo Shirika la Posta linaendelea kupiga hatua katika utoaji wa huduma zake.




*Kaimu Posta Masta Mkuu Bw. Macrice Mbodo (kushoto)katika Picha ya pamoja na Mtendaji Mkuu wa (UCSAF) Bi. Justina Mashiba(kulia)*



# MATUKIO KWA PICHA



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari  Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya kiutendaji kati ya Shirika la Posta na TanTrade.



Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Prof Kitila Mkumbo akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya kiutendaji kati ya Shirika la Posta na TanTrade.



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari  Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) akipokea bidhaa aliyonunua kupitia Duka Mtandao la Posta wakati wa  hafla ya utiaji saini  makubaliano ya kibiashara kati ya Shirika la Posta na TanTrade.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano Dkt Zainab Chaula akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano ya kibiashara kati ya Shirika la Posta na TanTrade.

# POSTA YASHIRIKI KONGAMANO LA 12 LA MWAKA LA WATAALAM WA MANUNUZI NA UGAVI

Shirika la Posta Tanzania ambalo ni miongoni mwa wadhamini wa Kongamano la 12 la mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi nchini limeshiriki Kongamano hili lililoanza tarehe 1 Disemba - 3 Disemba 2021 lililofanyika katika Ukumbi wa AICC jijini Arusha.

Shirika la Posta Tanzania limetumia jukwaa hilo kufanya wasilisho juu ya huduma na biashara mbalimbali zinazofanya na Shirika hilo hapa nchini. Wasilisho hilo limefanywa na Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji wa Biashara za Shirika Bwana Constantine Kasese kwa niaba ya Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo Bwana Macrice Daniel Mbodo.

Bwana Kasese ameelezea huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika la Posta nchini ikiwemo huduma za Usafirishaji wa barua na vipeto, huduma za Uwakala na Fedha ikiwemo "Bureau de Change", EMS pamoja na huduma nyingine nyingi.

Aidha Bwana Kasese ametumia jukwaa hilo kuelezea huduma mbalimbali zilizoboreshwa na Shirika hasa huduma za kidijitali ikiwemo huduma ya Duka Mtandao (Posta Online Shop) ambalo linawapa fursa wajasiriamali nchini na hata nje ya nchi kutangaza na kuuza bidhaa zao kupitia duka hilo lililounganishwa na nchi zaidi ya 192 zilizopo chini ya Umoja wa Posta Duniani (UPU) na hata kuwezesha watu wengi duniani kuagiza na kununua bidhaa popote walipo duniani.

Aliendelea kueleza kuwa huduma za kidijitali zilizoanzishwa na Shirika ni pamoja na huduma ya Posta Kiganjani (SmartPosta) inayomuwezesha mteja kufuatilia taarifa ya mzigo au barua anayotuma akiwa popote pale alipo. Alisema kuwa huduma hii inapatikana kwa kupakua "application" ya "SmartPosta" inayopatikana "Play Store" na baada ya hapo mtumiaji ataweza kujisajili ili kuanza kuitumia huduma hiyo.

Sambamba na hilo Bwana Kasese aliongeza kuwa Shirika la Posta nchini limeanzisha vituo vya "Huduma Pamoja" vinavyotoa huduma mbalimbali za Serikali katika ofisi za posta ambapo kwa awamu ya kwanza Shirika limeanzisha vituo hivyo kwenye mikoa wa Dar es Salaam na Dodoma.

Huduma zinazopatikana kwenye vituo hivyo ni pamoja na huduma za NSSF, PSSF, RITA, NIDA, BRELLA, TRA, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Jiji la Dodoma, CRDB na NHIF.




Posta
Let's Go!

# PICHA KWA MATUKIO




Mgeni rasmi wa Kongamano Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongela (aliyekaa wa nne kutoka kushoto) kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mpango Mhe. Dkt Mwigulu Nchemba akiwa katika picha ya pamoja na wadhamini wa Kongamano hilo. Waliosimama wa pili ni Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji wa Biashara za Shirika la Posta Tanzania Bwa. Constantine Kasee.




Baadhi ya watumishi wa Shirika la Posta Tanzania waliokuwa wakitoa huduma katika Banda la Shirika la Posta lililokuwa katika viwanja vya Kongamano Jijini Arusha.

# PONGEZI KWA UTEUZI



**Mhe. Nape Nnauye(Mb)**
**Waziri wa Wizara ya Habari,**
**Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**



**Mhe. Mhandisi Kundo Mathew(Mb)**
**Naibu waziri wa Wizara ya Habari,**
**Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**



**Dkt. Jim James Yonazi**
**Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari,**
**Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**



**Bw. Mohamed Khamis**
**Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari,**
**Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

# MAJALIWA AZITAKA TAASISI ZA SERIKALI KUJIUNGA NA KUTUMIA HUDUMA PAMOJA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amezielekeza taasisi zinazotoa huduma za Serikali kwa wananchi kuongeza kasi ya kujiunga na kutumia Huduma Pamoja iliyopo ndani ya Shirika la Posta Tanzania.

Hayo ameyasema siku ya jumatatu tarehe 6, Septemba 2021 wakati akizungumza na viongozi mbalimbali na wananchi waliohudhuria uzinduzi wa vituo vya Huduma Pamoja utakayo jumuisha taasisi mbalimbali za Serikali ili kutoa huduma zake ndani ya ofisi za Shirika la Posta nchi nzima.

Akizungumzia huduma hiyo, Mhe. Majaliwa alisema kuwa Huduma Pamoja ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa Serikali ambapo lengo kuu ni kuweka mazingira rahisi na wezeshi kwa wananchi kupata huduma zote za Serikali ndani ya eneo moja na kwa muda mfupi.

"Maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano yameongezeka na kuanzishwa kwa huduma hii kutasaidia kupunguza msongamano na usumbufu kwa wananchi na utakapofika mwaka 2025 tunaamini mageuzi haya yatakuwa katika vituo vyote 350 vya Shirika la Posta nchini". amesema.




Aidha, Mhe. Majaliwa ameipongeza Wizara ya Mawasiliano na Teknolojla ya Habari chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile na Katibu Mkuu, Dkt. Zainab Chaula za kwa juhudi na usimamizi mahiri wa taasisi mawasiliano ikiwemo Shirika la Posta nchini hata kupelekea utekelezaji wa mradi wa kitaifa wa Serikali wa Huduma Pamoja wenye lengo la kuweka mazingira rahisi na wezeshi kwa wananchi kupata huduma zote za Serikali katika jengo moja.

Ameeleza kuwa Serikali inaendelea kufanya maboresho mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapitio ya sera na sheria za Posta ili kuendana na mahitaji ya soko na matarajio ya wananchi lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa mageuzi yanayofanyika katika Sekta ya Mawasiliano nchini yanakuwa na tija katika utoaji huduma hususan huduma za Posta.




Posta Let's Go!

# MAJALIWA AZITAKA TAASISI ZA SERIKALI KUJIUNGA NA KUTUMIA HUDUMA PAMOJA

Pia, Waziri Mkuu amemtaka Mhe. Dkt. Ndugulile kama msimamizi wa mradi huo kupitia Wizara yake kuongeza kasi ya utekelezaji ilü kuharakisha utatuzi wa changamoto zinazowakabili wananchi katika kupata huduma za Serikali na kuhamasisha ubunifu na utafiti katika Sekta ya Posta na TEHAMA ilikuleta mapinduzi ya bidhaa na huduma kwa maisha bora yawananchi.

Sambamba na hilo, Mhe. Waziri Mkuu amelitaka Shirika hilo kutumia fursa hiyo kusimamia uendeshaji wa huduma zote za pamoja zinazotolewa kupitia Ofisi zake kuwa zinatolewa kwa weledi na ufanisi ili kuepuka kuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya upatikanaji wa huduma hizo katika hatua za mwanzo za uanzishwaji wa huduma hi.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amempongeza Dkt. Faustine Ndugulile kwa kuweza kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania duniani kupitia Shirika la Posta Tanzania kufuatia kushinda nafasi mbili kwa Tanzania kuwa mjumbe wa Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani katika chaguzi zilizofanyika katika Mkutano Mkuu wa 27 wa Umoja wa Posta Duniani nchini lvory Coast mwezi Agosti, 2021.

Mhe. Majaliwa ameielekeza ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambacho ni chombo kinachosimamia utoaji wa huduma za Serikali kuhakikisha taasisi zinazotoa huduma za Serikali katika vituo vya Huduma Pamoja mpaka ifikapo mwaka 2022 ziwe zimejiunga na Huduma Pamoja ili kukidhi matarajio ya Serikali kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi wake.

Pia, ametoa maelekezo kwa Wizara zote nchini zinazosimamia taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi kuhakikisha taasisi hizo zinajiunga na kutumia Huduma Pamoja na kuanza kutoa huduma zake kupitia vituo vya Huduma Pamoja ili wananchi wapate huduma husika kwa urahisi na kwa wepesi
.

Naye Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt Faustine Ndugulile ameelezea kuridhishwa kwake na kasi ya utendaji wa Shirika hilo na kupongeza jitihada na juhudi zinazofanywa na Kaimu Postamasta Mkuu bwana Macrice Mbodo kwa kulifanya Shirika hilo kuwa posta ya kisasa.

Aidha, ameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Shirika hilo shilingi bilioni 3.9 ambazo zilitumiwa na Shirika hilo kulipa wastaafu wa liliyokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki na kuahidi kuzielekeza fedha hizo kuifanya Posta ya kidijitai kwa kununua nyenzo zitakazoongeza kasi ya utendaji ya Shirika la Posta nchini.

Dkt. Ndugulile alieleza kuwa mkakati wa Wizara yake ni kujikita katika kulifanya Shirika la Posta kuwa kitovu cha Biashara Mtandao duniani kwani Posta ina mtandao mpana ambao unaunganisha posta zaidi ya 600,000 duniani utakaowezesha wajasiriamali kuuza bidhaa zao mahali popote duniani.

"Tunataka Shirika letu la Posta liwe kitovu cha biashara mtandao kwani tunafahamu uaminifu umekuwa ni changamoto sana lakini kupitia Shirika letu la Posta tunataka kujenga uaminifu huo ili kila mwananchi anufaike na duka hili"



# MAJALIWA AZITAKA TAASISI ZA SERIKALI KUJIUNGA NA KUTUMIA HUDUMA PAMOJA

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya-Bunge ya Miundombinu Bw. Selemani Kakoso ameishukuru Serikali kwa kuliwezesha Shirika la Posta nchini kuanzisha huduma hii na ametoa wito kwa watumishi wa umma kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi pamoja na kufuata taratibu za utumishi wa umma ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa upande wake Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo Bw. Macrice Daniel Mbodo amesema bado Shirika linaendelea kuboresha huduma na kwa sasa linaendelea kutengeneza faida na kwa mwaka wa fedha ulioisha limeingiza faida ya shilingi bilioni 3 na mabadiliko ya mfumo wa kidijitali yataenda kwa awamu tatu ambapo kufikia Desemba 2022 mikoa 10 itakuwa imepata Huduma Pamoja kwa huduma zote za Serikali kupatikana katika ofisi moja.

Tunaanza na mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma, tutaenda Mwanza, Kigoma, Arusha, Mbeya, Zanzibar, Mjini Magharibi, Chakechake Pemba, Lindi, Tanga na Morogoro na awamu ya pili itaanzia mwaka 2023/24 na itakuwa katika mikoa ya Pwani, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Kilimanjaro, Tabora, Mara, Kagera, Shinyanga, Lindi, Simiyu, Mtwara, Manyara, Songwe, Katavi, Njombe na Geita amesema Mbodo




Aidha, ameongeza na kusema kufikia Desemba 2025 Shirika la Posta limejidhatiti kufikisha Huduma Pamoja kwa ngazi ya Wilaya ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Naye Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika bwana

Sifundo Chief Moyo ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuboresha Sekta ya Posta nchini kwani maboresho hayo yatachochea maendeleo katika Taifa hasa katika kipindi hiki cha maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Pia, ameihakikishia Serikali ya Tanzania ushirikiano wa kutosha katika kuifanya Sekta ya Posta kuwa ya kidijitali.

Baadhi ya taasisi za Serikali ambazo zinatoa huduma ndani ya Shirika la Posta ni NSSF, PSSF, RITA, NIDA, BRELLA, TRA, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Jiji la Dodoma CRDB na NHIF.



# MHANDISI KUNDO AZINDUA DUKA LA POSTA MTANDAO

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhandisi Kundo Mathew amezungumzia huduma ya duka la posta mtandao kuwa ni moja ya ubunifu wa biashara uliofanywa na Shirika la Posta Tanzania ikiwa ni matokeo ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Mhandisi Kundo alizungumza hayo tarehe 06/10/2021 wakati wa uzinduzi rasmi wa duka la posta mtandao jijini Dodoma sambamba na uzinduzi wa maonesho ya Wiki ya Posta kuelekea Siku ya Posta duniani itakayofanyika tarehe 9/10/2021

Amesema kuwa kupitia Duka la Posta mtandao wajasiriamali na wafanyabiashara waliopo nchini wataunganishwa na masoko ya biashara na bidhaa zao pote duniani kupitia matawi ya Shirika la Posta duniani pote na matawi zaidi ya 350 ya Shirika la Posta yaliyopo ndani ya nchi.

"Duka la Posta Mtandao limedhihirisha kwa vitendo ubunifu mkubwa wa watendaji wa Wizara na taasisi katika kutafsiri Sera ya TEHAMA na kuleta mapinduzi makubwa ya teknolojia ya kidijitali katika utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao". alisemaa Mhandisi Kundo





"Ubunifu uliofanywa na Shirika hilo umeleta mapinduzi makubwa ya kuuza na kununua bidhaa pote duniani ambapo mpaka sasa wajasiriamali wapatao 428 nchini wamesajiliwa na duka hilo". aliongeza Injinia Kundo

Kwa upande wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Zainab Chaula amesema kuwa Wizara hiyo na taasisi zake inatembea na kauli mbiu ya kutembea pamoja na kazi yao kubwa ni kuweka miundombinu itakayoifikisha nchi kwenye uchumi wa kidijitali kupitia Wizara hiyo na taasisi zake.

Amesema kuwa kuna mafanikio mengi yaliyopatikana kupitia Shirika la Posta Tanzania mojawapo ni kupata uwakilishi wa mabaraza mawili ya Umoja wa Posta Duniani ambayo ni Mjumbe wa Baraza la Utawala na Mjumbe wa Baraza la Uendeshaji la umoja wa Posta Duniani wenye jumla ya nchi wanachama 192

Posta
Let's Go!

# MHANDISI KUNDO AZINDUA DUKA LA POSTA MTANDAO




Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Dkt. Jabir Kuwe amesema kuwa Shirika la Posta limeonesha kuwa teknolojia ni fursa kwa mabadiliko makubwa yaliyoonekana baada ya Shirika hilo kuanza kutumia teknolojia kwenye utoaji wa huduma zake ambapo mpaka sasa jumla ya leseni 119 zimetolewa na TCRA katika Sekta ya Posta.

Kaimu PostaMasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo amesema kuwa Shirika la Posta la sasa ni zaidi ya kutuma na kupokea barua na kuwataka wananchi kujiunga na Duka la Posta Mtandao kupitia tovuti ya www.postashoptz.post.

Amezitaja sifa kubwa za duka hilo kuwa limeunganishwa na mtandao mpana wa Posta duniani, linatumia lugha zaidi ya 20, lina huduma za usafirishaji wa haraka na wa njia ya kawaida, uhakika wa masoko ya ndani na nje ya nchi na asilimia 97 ya mauzo inabaki kwa mfanyabiashara au mjasiriamali.

Posta
Let's Go!

# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAINGIA MAKUBALIANO NA BENKI YA CRDB




Benki ya CRDB imezindua upya huduma za CRDB wakala kupitia Shirika la Posta Tanzania kwa ajili ya kuwezesha wateja na watanzania wote kwa ujumla kupata huduma za benki hiyo kwa urahisi na unafuu. Hafla ya uzinduzi ilifanyika katika makao makuu ya posta jijini Dar es salaam na kuhudhuriwa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya habari, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile pamoja na viongozi mbalimbali wa Taasisi hizo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Ndugulile alisema kuwa ubia huo wa Benki ya CRDB na Posta utasaidia kuongeza ujumuishi wa kifedha nchini kwa kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Aidha alibainisha kuwa Serikali kupitiaa mpango wa tatu wa Maendeleo wa miaka mitano imejipanga kuhakikisha matumizi ya njia mbadala za kutoa huduma za kifedha yanaongezeka ili kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan waliopo vijijini.

*"Nimefurahishwa sana kuona benki ya CRDB ikiwa mstari wa mbele katika eneo hili, kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika mifumo ya kidijitali ya kutolea huduma ikiwamo CRDB wakala. Niwaombe mkasimamie vizuri ubia huu ili huduma zinazotolewa zikawe na manufaa kwa watanzania wengi"* alisema waziri Ndugulile.

Waziri Ndugulile aliwataka wananchi kutumia vizuri fursa hiyo ya CRDB wakala kupitia Shirika la Posta kupata huduma za kibenki hasa ukizingatia kuwa Shirika hilo lina ofisi kwenye wilaya zote nchi nzima. "Ripoti ya ujumuishi wa fedha inayooshesha ni asilimia 16.7 tu ya watanzania wote ambao wanapata huduma za benki.

*"Tukiitumia fursa hii vizuri tutakwenda kuongeza idadi ya watanzania waliounganishwa katika mfumo rasmi wa kifedha",* alisisitiza huku akiwataka Benki ya CRDB na Shirika la Posta kutoa elimu ya kutosha juu ya huduma hiyo.

Posta
Let's Go!

# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAINGIA MAKUBALIANO NA BENKI YA CRDB

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Bw. Abdulmajid Nsekela alimweleza waziri Ndugulile kuwa kupitia ubia huo Benki ya CRDB itatumia ofisi zaidi ya 100 za Shirika la Posta kufikisha huduma za kifedha kwa wateja wake kwa kutumia mfumo wa CRDB Wakala.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, alisisitiza kuwa uzinduzi wa huduma hiyo ni sehemu ya mkakati wa Benki hiyo kubuni namna bora ya kufikisha huduma kwa wateja ili kusaidia jitihada za Serikali katika kuongeza ujumuishi wa kifedha.

"Niwakaribishe wateja wetu wote nchi nzima na hata wale wasio wateja kupata huduma zetu kupitia Shirika la Posta kwani huduma zote zinapatikana kupitia madirisha ya CRDB Wakala" aliongeza Nsekela huku akibainisha kuwa kupitia ubia huo wateja wataweza kunufaika na huduma nyingi za benki hiyo ikiwamo kufungua akaunti, kuweka na kutoa fedha, kulipia ankara, kulipa tozo na kodi za Serikali, kulipia bima na huduma nyengine nyingi za kibenki.

Akieleza mafanikio ya CRDB Wakala tokea kuanzishwa kwake mwaka 2013, Nsekela alisema mpaka sasa Benki hiyo in mawakala zaidi ya 20,000 waliosambaa kote nchini mijini na vijijini. Alibainisha zaidi kuwa mfumo huo umesaidia kupunguza gharama ya kufikisha huduma kwa wateja lakini pia kutoa ajira kwa watanzania na hivyo kukuza kipato cha wananchi.

*"Najivunia kusema nimepata mafaniklo makubwa sana kupitia mfumo huu wa CRDB Wakala, sasa hivi zaidi ya asilimia 40 ya miamala ya wateja hufanyika kupitia CRDB Wakala kulinganisha na matawi"* alisema Nsekela.

Naye Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta, Bwana Macrice MBodo alimhakikishia Waziri Ndugulile kuwa Shirika limejipanga kikamilifu katika kuhakikisha malengo ya ubia huo.

*"Tunajivunia kuwa sehemu ya suluhisho la upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi. Nikuahidi mheshimiwa Waziri tutasimamia vizuri utoaji wa huduma kwa wateja ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa urahisi na haraka"* alisema Bwa. Mbodo huku akiishukuru Benki ya CRDB kwa mafunzo ambayo wameyatoa kwa wafanyakazi wa Shirika, ili waweze kutoa huduma kwa weledi na kwa ufanisi.



Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania wakisikiliza hotuba mbalimbali katika hafla hiyo

# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA KUSHIRIKIANA NA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR




Shirika la Posta Tanzania katika kuendelea kuboresha huduma zake Tanzania Bara na Visiwani, limetiliana saini ya mashirikiano ya kibiashara na Shirika la Bima la Zanzibar.

Hafla ya utiaji wa saini ilifanyika kwenye ofisi za Makao Makuu ya Shirika la Bima la Zanzibar tarehe 15 Julai 2021. Mgeni Rasmi katika Hafla hiyo alikuwa Dk. Juma Malik Akili Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Juma Malik Akili ametoa pongezi za dhati kwa mashirika yote mawili Shirika la Posta Tanzania pamoja na Shirika la Bima Zanzibar kwa kuiona fursa itakayopelekea kuihudumia jamii kwa urahisi na kwa wepesi
.

Nae Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bima Zanzibar amesema kuwa Shirika la Bima la Zanzibar lipo tayari kufanya kazi na Shirika la Posta kwani Mashirika yote ni ya Serikali na ni fursa kwa Shirika la Bima la Zanzibar kueneza huduma kwa Upande wa pili wa JMT

Aidha Kaimu Postamasta Mkuu Ndugu Macrice Daniel alieleza kuwa Shirika la Posta kwa sasa linaendelea kuboresha huduma zake lengo ni kumfanya Mwananchi apate huduma bora kutoka katika Shirika hilo.

Mkataba huo wa mashirikiano ya kibiashara utawawezesha Wananchi kupata Bima kupitia Ofisi za Shirika lao la Posta Tanzania lililo na matawi nchi nzima

# UCHUMI WA KIDIJITALI NDIO MKAKATI WA NCHI KWA SASA - NDUGULILE

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya habari, Mhe. Dkt.Faustine Ndugulile (Mb) ameeleza kuwa *kwa sasa mkakati wa nchi ni kuelekea kwenye uchumi wa kidijitali 'Digital Economy' hivyo mashirika ya umma yanatakiwa kuwa mstari wa mbele kupokea na kutelekeza mabadiliko haya kwa manufaa ya Taifa na jamii ya watanzania kwa ujumla.*

Maneno hayo ameyasema wakati akishuhudia utiaji saini na makubaliano ya kibiashara baina Shirika la Posta Tanzania na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) yaliyofanyika tarehe 7 Julai 2021, kwenye viwanja vya maonesho ya kibiashara ya sabasaba Jijini Dar es salaam.




Dkt Ndugulile amelipongeza Shirika la Posta na TANTRADE kwa maono haya ya kuitumia teknolojia kwa ajili ya kuinufaisha jamii huku ikiwaunganisha wafanyabiashara eneo moja na kuwatambulisha katika soko la ndani na nje ya nchi kupitia Duka mta ndao la Posta

*"Duka hili litamwezesha mteja kuuza, kutangaza na kununua bidhaa tofauti tofauti ndani na nje ya nchi kwa njia ya mtandao.Miamala ndani ya duka hili itafanyika mtandaoni, baada ya kujisajili kupitia tovuti rasmi ya duka hili ambayo ni www.postashoptz .post ".* Alifafanua Dkt. Ndugulile.




Aidha, Dkt Ndugulile ameutaka uongozi wa Shirika la Posta Tanzania kulinganisha duka hili la mtandao na maduka mengine ya mtandao ya Posta zingine Duniani ili kuongeza soko la bidhaa za Tanzania nje ya Nchi.

Nae Waziri wa viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo amempongeza Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe Dkt Faustine Ndugulile na Katibu Mkuu wake, Dkt. Zainabu Chaula, kwa kazi kubwa wanayoifanya ndani ya Wizara hiyo, huku akisisitiza kuwa, katika mabadiliko ya kihuduma yanayofanywa ndani ya Shirika la Posta, yasiondoe huduma nzuri za zamani za shiriika hilo kama utumaji wa barua kwenye sanduku la barua ili kuifanya Posta ibaki na uhalisia wake.

Naye Kaimu Postamasta Mkuu, Bw Macrice Daniel Mbodo alieleza mabadiliko mbalimbali ya kihuduma yanayofanywa ndani ya Shirika la Posta hasa kwenye eneo la kidijitali na matumizi ya Duka Mtandao la Posta na namna ya kujiunga na duka hilo.

## BAADHI YA MAGARI YA SHIRIKA YANAYO TUMIKA KATIKA SHUGHULI ZA USAFIRISHAJI






# WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHE. DKT. FAUSTINE NDUGULILE (MB), APEPERUSHA BENDERA YA TANZANIA KIMATAIFA

Umoja wa Posta Duniani(UPU) umetumia Mkutano Mkuu wa 27 kuwakutanisha Mawaziri wenye dhamana ya Sekta ya Posta katika Kongamano la kujadili mwelekeo wa Posta Kimataifa na mageuzi katika utoaji wa huduma za Posta.

Mjadala huu ulihusu : *UVIKO-19 na Sekta ya Posta Nini kimebadilika, Nini hakijabadilika, Nini kibadilike" na mchango wa Jumuiya za Kimataifa hasa UPU* .

Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, aliongoza mjadala wa Mawaziri katika Kongamano hilo Akiangazia Nini kifanyike kwa Jumuiya za kimataifa hasa kwa Umoja wa Posta Duniani katika kuwezesha mageuzi makubwa kwa mashirika ya Posta Duniani kutoa huduma kwa ufanisi hata katika kipindi hiki cha janga la UVIKO-19.

Alisema pamoja na janga la UVIKO-19 huduma za Posta bado zipo, Posta zinahitajika kubadili namna ya utoaji wa huduma na pia kusisitiza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za Posta.

Alieleza kuwa ni muhimu UPU kusaidia nchi wanachama katika maeneo ya:

Uwekezaji katika maeneo ya Teknolojia, matumizi ya mifumo ya TEHAMA unganishi; Kubadilishana uzoefu miongoni mwa nchi wanachama; kuwa na kanuni bora za uthibiti ili kukuza biashara za kupitia mipakani kutokana na ukuaji wa biashara mtandao; na kuwezesha utoaji wa huduma katika eneo moja (Huduma Pamoja).

Akifungua Kongamano Hilo *Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Ivory Coast Mhe. Patrick Achi* alisema kuwa kuna umuhimu wa kuikuza Sekta ya Posta Duniani Ili kusiwe na tofauti kati ya Kaskazini na Kusini mwa jangwa la sahara jambo ambalo amesisitiza lizingatiwe wakati wa kujadili na kupitisha Mkakati wa Posta wa Dunia ( Abidjan World Postal Strategy 2022-2025) Ili Mkakati huo uweze kuipeleka mbele Sekta ya Posta.

Hili ni kongamano la nne tangu kuanza kwake mjini Doha, Qatar 2012, likifuatiwa na Istanbul, Uturuki mwaka 2016 na lile la Addis Ababa, Ethiopia mwaka 2018.




Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akiongoza mjadala wa Mawaziri katika Kongamano hilo.

# TANZANIA YANG'ARA UCHAGUZI WA MABARAZA YA UMOJA WA POSTA DUNIANI (UPU)


Tanzania ilifanikiwa kupeperusha vema bendera yake kwenye Mkutano Mkuu wa 27 wa umoja wa Posta Duniani uliofanyika jijini abidjan, Ivory coast, baada ya kuibuka kid-edea katika uchaguzi wa Mabaraza ya Utawala (Council of Administration) na lile la uendeshaji (Council of Operation) la umoja huo

Tanzania ilifanikiwa kuingia katika Baraza la Utawala kutoka kundi la Afrika lenye nchi 54 na zilitakiwa nchi 11kuiwakili-sha Africa katika kwenye baraza hilo. Pia Tanzania ilifanikiwa kuingia kwenye Baraza la uendeshaji la Umoja huo ambalo lilikuwa na ushindani mkubwa. Tanzania iliibuka kati ya nchi zilizopata uungwaji mkubwa wa nchi 123. Hii inafanyika Tanzania kuwa na nafasi mbili muhimu katika uendeshaji wa shughuli za Umoja huo.

Hii ni historia kubwa katika historia ya sekta ya Posta nchini Tanzania ambapo kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa Umoja huo mwaka 1874 Tanzania haijawahi kuwa mjumbe wa Mabaraza yote mawili kwa wakati mmoja




Kaimu Postammasta Bw. Mkuu Macrice Mbodo akipiga Kura wakati wa mkutano huo.



Waziri wa Mawasiliano Teknolojia ya Habari Mh. Daktari. Faustine Ndugulile (Mb) Katika Mkutano Mkuu wa 27 wa Umoja wa Posta Duniani jijini Abidjan, Ivory Coast.

Posta
Let's Go!

# MBODO: JIANDAE KIKAMILIFU MNAPOSHIRIKI VIKAO



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bwa. Macrice Daniel Mbodo amelitaka Baraza la majadiliano la Shirika la Posta nchini kufanya majadiliano kwa weledi na kujiandaa kikamilifu pindi wanaposhiriki majadiliano hayo ili kuleta tija ya majadiliano hayo kwa Shirika.

''Mjiandae kikamilifu na majadiliano kabla ya kukutana kwenye vikao, sheria imesisitiza tusiingie tu kwenye vikao na kuanza kutunga agenda zingine, kwa maana maandalizi yanapaswa kufanywa kabla.'' Alisema Bw. Mbodo

Haya aliyasema wakati alipokuwa akifungua rasmi kikao cha Baraza la Majadiliano kinachofanyika katika ukumbi wa Beda, Mjini Morogoro na kuhudhuriwa na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na Menejimenti ya Shirika hilo.

Aidha, Kaimu Postamasta Mkuu alitumia nafasi hiyo kutoa taarifa ya maendeleo ya Shirika kwa ujumla na mikakati ya Shirika ya kuongeza biashara ili kuhakikisha linatoa huduma stahiki kwa wananchi.

Moja kati ya taarifa hizo ni kulifahamisha Baraza hilo kuwa Serikali Kupita Wizara ya Fedha na Mipango nchini imelipatia Shirika la Posta kiasi cha shilingi Bilioni 3.9 kati ya Bilioni 7.9 zilizotumiwa na Shirika kulipa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika mashariki

Bw. Mbodo aliwafahamisha wajumbe kuwa tayari Shirika limeshapeleka mapendekezo kwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari namna ambavyo litazitumia fedha hizo kuboresha na kuongeza vitendea kazi ikiwemo magari, pikipiki kompyuta na kuboresha mifumo yake ili kulifanya Shirika kuwa la kidijitali kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuwahudumia wananchi wengi kwa wakati mmoja.

''Serikali kupitia wizara ya fedha imeshalipatia Shirika la Posta kiasi cha Shilingi bilioni 3.9 na tayari tumewasilisha mapendekezo Wizarani ya namna ambavyo fedha hizo tutakwenda kuzitumia lakini sehemu kubwa ya matumizi ya fedha hizo ni kuboresha vitendea kazi ikiwemo magari, kompyuta ili wafanyakazi wa Posta waweze kufanya kazi katika mazingira rafiki''. Alisema Bw. Mbodo.

# MBODO: JIANDAE KIKAMILIFU MNAPO SHIRIKI VIKAO

Hata hivyo Bw. Mbodo alitumia fursa hiyo kuwajulisha wajumbe wa baraza hilo namna ambavyo Shirika la Posta limefanikiwa kuiwakilisha vyema nchi ya Tanzania kwa kufanikiwa kushinda nafasi mbili kwenye uchaguzi wa wajumbe wa Mabaraza ya Umoja wa Posta Duniani kwenye Mkutano wa 27 wa Umoja huo uliofanyika nchini Ivory Coast mwezi Agosti, 2021.

Katika mkutano huo Tanzania imeshinda nafasi ya kuwa mjumbe wa Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani. Pia Tanzania imefanikiwa kuwa Mwenyekiti mwenza wa kamati inayohusiana na biashara mtandao.

Kaimu Postamasta Mkuu alieleza mkakati wa Serikali kwa Shirika la Posta kupitia mradi wa Vituo vya "Huduma Pamoja" ambapo mpaka sasa zimetengwa kiasi cha shilingi Bilioni 50 kuwezesha mradi huo ambao utawawezesha wananchi kupata huduma zote za Serikali kwenye eneo moja kwa wepesi na uharaka zaidi.

Aidha, Bw. Mbodo alipata nafasi ya kueleza mkakati wa kuifanya Siku ya Posta Duniani ambao huadhimishwa kila mwaka tarehe 9 Oktoba kuwa ya kipekee, ambapo kwa mwaka huu mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango. Pia siku hiyo itaambatana na wiki ya posta.

Katika hatua nyingine, Kaimu Postamasta Mkuu ameeleza mwelekeo wa Shirika wenye kuifanya posta kuwa ya kidigitali [Digitalization] ambapo Shirika litajikita zaidi kwenye Biashara Mtandao [E-Commerce] na kuimarisha huduma za usafirishaji kwa kuimarisha Kitengo cha usafirishaji kuwa Kitengo kinachojitegemea na kutafuta biashara ili kuongeza pato kwa Shirika.

Pia, alieleza namna ambavyo Shirika linaendelea kukuza mahusiano ya kibiashara na Mashirika na Taasisi mbalimbali nchini ambapo mpaka sasa Shirika limejenga mahusiano mazuri ya kibiashara na Shirika la Ndege nchini [ATCL], NMB, Benki ya mkombozi, CRDB, Mamalaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), NBC na nyingine nyingi, lengo ikiwa ni kuwafikia wananchi wengi kwa wakati.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Bw. Omari M. Dibibi amempongeza Kaimu Postamasta Mkuu kwa utendaji wake na amemshukuru kwa kukubali kufungua kikao hicho na kumuahidi kuendesha mkutano huo kwa weledi ili kuleta matokea chanya ndani ya Shirika kama ilivyokusudiwa.

Kwa upande wa Msemaji Mkuu wa Wafanyakazi Junus Ndaro alipongeza juhudi zilizofanyika na mikakati mizuri inayoonekana ya kuboresha utendaji wa Shirika ikiwa ni sehemu ya kuliboresha Shirika la Posta nchini kwa maslahi mapana ya Taifa letu.



Posta
Let's Go!

# Posta Kiganjani

Twen'zetu Kidigitali!

## Pata Sanduku lako chap !

Kupitia app yetu ya SmartPosta

**Jisajili**

Posta Let's Go!

# SERA YA MAZISHI NA UKIMWI KUWASILISHWA KWENYE BARAZA LA MAJADILIANO LA TPC

Mwenyekiti wa Baraza la Majadiliano la Shirika la Posta Tanzania Omari M. Dibibi amefunga rasmi kikao cha majadiliano ya maslahi ya wafanyakazi wa Shirika la Posta na kufikiwa maamuzi ya kuwasilishwa katika Baraza la majadiliano la Shirika hilo.

Kikao hicho kilichofunguliwa na Kaimu Postamasta Mkuu Bw. Macrice Mbodo kilipata wasaa wa kuangalia kwa undani maslahi mapana ya wafanyakazi wa Shirika kuhusiana na sera ya UKIMWI na mazishi kwa wafanyakazi.

Baada ya majadiliano ya siku mbili, Kikao hicho kimefungwa rasmi huku kikihudhuriwa na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, Menejimenti na wawakilishi wa Menejimenti ya Shirika la Posta nchini, katika ukumbi wa Edema, Mkoani Mororgoro.

Baraza hilo limeweza kupokea sera mbili zilizowasilishwa na menejimenti ya Shirika zinazohusiana na masuala ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI pamoja na masuala yanayohusu mazishi kwa wafanyakazi wa Posta, lengo likiwa ni kuweka mazingira rafiki kwa watendaji wa Shirika hilo nchini.

Aidha, sera hizo zinaenda kuleta usawa kwa wafanyakazi wa Shirika la Posta bila kuzingatia dini wala vyeo katika masuala yote yatakayo husiana na misiba.

Vilevile kupitia Baraza hilo, Menejimenti ya Shirika imewasilisha pia sera ya UKIMWI ambayo inaitaka Shirika kuwapa elimu wafanyakazi namna ya kujikinga na kujilinda na maambukizi hayo.

Sambamba na hilo, sera hiyo imelitaka Shirika la Posta kuweka mazingira wezeshi kwa watendaji wake wanaoishi na magonjwa hayo.

Posta
Let's Go!





# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA NA MIKAKATI YA KUKUZA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice mbodo Alipata wasaa wa kukutana na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye ukumbi wa mikutano wa Peoples Palace, Mjini Zanzibar.

Kwenye kikao hicho, kilichoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Said, Kaimu Postamasta Mkuu alielezea Shirika lilikotoka, lilipo sasa na mwelekeo wake wa baadaye katika kuwezesha upatikanaji wa huduma bora na zenye tija kwa Taifa na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Bluu Zanzibar.

Bw. Mbodo alifafanua kuwa huduma za usafirishaji, huduma ya Duka Mtandao la Posta, huduma za uuzaji na usambazaji wa stempu hasa zenye historia na vivutio mbalimbali nimaeneo ya kimkakati ambayo shirika linayaangalia kwa umakini mkubwa na ni chanzo kikubwa cha mapato visiwani Zanzibar

Sambamba na hilo, Bw. Mbodo alieleza kuwa, Shirika la Posta Tanzania linaendelea kuboresha utoaji wa huduma hizo ili wananchi wa pande zote za Muungano waweze kunufaika na huduma hizo.

Hivyo Bw. Mbodo aliwaomba wajumbe wa Baraza la Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendelea kuhamasisha wananchi wa Zanzibar kwa kutumia huduma za Posta ili kuchangia pato la Taifa na hatimaye kukuza uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa Ujumla.

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta pia alipata nafasi adhimu ya kukabidhi Zawadi ya saa maalumu kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Said yenye Nembo ya Shirika la Posta, picha za stempu zenye vivutio vilivyopo Zanzibar, picha ya magari kuonesha huduma ya usafirishaji, na Duka mtandao la Shirika ikiwa ni sehemu ya huduma za Shirika la Posta zenye lengo la kukuza maendeleo ya uchumi wa buluu Zanzibar.



# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA NA MIKAKATI YA KUKUZA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR



Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Said (kushoto) akiifurahia saa maalum aliyokabidhiwa kama zawadi na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo (Kulia), visiwani Zanzibar




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo (Kulia) akikabidhi saa maalum kwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Said (kushoto)

# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAKUTANA NA JUKWAA LA WAHARIRI NCHINI

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo, tarehe 29 Julai 2021 amekutana na kufanya mazungumzo na jukwaa la wahariri na waandishi wa habari nchini, lengo ikiwa ni kuwafahamisha mwelekeo wa Shirika la Posta tangu kuanzishwa kwake hadi sasa.

Kaimu Postamasta Mkuu alitumia nafasi hiyo kuelezea mwelekeo wa shirila ambao umejikita katika kulifanya Shirika la Posta kuwa la kisasa zaidi kwenye eneo la utoaji wa huduma zake, ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

*"Tumeona ni vyema tuwaite wahariri ili tukae nao, tuzungumze nao, ili wajue Shirika limetoka wapi, liko wapi na nini mwelekeo wake tumeangalia tumepima na kuona ipo haja ya kuyaeleza haya mbele zenu ili myafikishe kwenye jamii kwa kutumia vyombo vyenu mlivyonavyo ili basi yafahamike na umma".*

Tunavyo vipaumbele tunavyovitekeleza kwa sasa ikiwemo uanzishwaji wa Duka mtandao, utoaji wa huduma za Serikali mahali pamoja kupitia ofisi za Posta(one stop centre), kuhakikisha Shirika linatoa huduma zake kidijitali kupitia simu janja, ambapo wananchi wataweza kupata huduma zote za Posta kupitia simu zao za mkononi, kwa kupakua "Application" ya "SmartPosta" inayopatikana Play Store

*"Posta tunayo ijenga ni Posta ambayo huduma zake zinapatikana kwa urahisi zaidi kupiti simu ya mkononi,* na kauli mbiu yetu tunasema Posta Kiganjani twenzetu kidijitali" Aliongeza Bw. Mbodo.



*Kaimu Postamasta Mkuu Ndg Macrice Mbodo akiongea na waliohudhuria kikao cha jukwaa la wahariri na waandishi wa habari nchini Tarehe 29 Julai 2021*

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri nchini, Deogratus Balile, aliwaasa wananchi kulitumia Shirika la Posta vizuri katika kupata huduma mbalimbali kwani Shirika hilo kwa sasa limeboresha sana huduma zake.

Hata hivyo Balile aliongeza kuwa, wafanyabiashara nao wanapaswa kulitumia vizuri Duka Mtandao la Posta kwa kuhakikisha kuwa taarifa walizosajili humo ni sahihi juu ya biashara ili waweze kuuza kirahisi.

Mkutano huo ulifanyika tarehe 29 Julai 2021, jengo la NSSF jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Menejimenti ya Shirika hilo.

Posta
Let's Go!

# DKT. NDUGULILE: NATAKA KUONA POSTA YA KIDIJITALI

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) amelitaka Shirika la Posta Tanzania kuwekeza kwenye mifumo ya kidigitali katika utoaji wa huduma zake hasa katika kipindi hiki ambacho dunia inapitia mabadiliko makubwa ya Sayansi na Teknolojia.

Hayo aliyasema tarehe 05 Agosti, 2021 wakati wa kufungua kikao kazi cha viongozi wa Shirika la Posta kwa ngazi Menejimenti na Viongozi wa Mikoa ya Posta nchini. Kikao hicho kililenga kutathmini utendaji kazi wa Viongozi hao kwa mwaka uliopita 2020/2021 na kukubalina malengo mapya kwa ajili ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Dkt. Ndugulile alisisitiza kuwa katika Dunia ya sasa watumiaji wa huduma za mtandao upande wa TEHAMA wameongezeka, hivyo Posta lazima iwekeze zaidi kwenye TEHAMA ili kuboresha utoaji huduma zake ili kuvutia jamii kutumia huduma za Posta.

Aidha, Dkt. Ndugulile alilitaka Shirika la Posta kuwa la kisasa zaidi kwa kuwekeza kwenye mifumo na utoaji wa huduma zenye ubora (Quality Management System) zinazoendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia ili kufikia viwango vya kimataifa vya utoaji wa huduma hizo zikiwemo Huduma ya Duka Mtandao, huduma za Kifedha na Uwakala, Huduma Pamoja na Posta Kiganjani.

Vilevile Mhe. Waziri alionyesha kufurahishwa na uanzishwaji wa Duka mtandao la Posta (E-Shop) ambalo linawapa fursa wafanyabiashara na wananchi wote kuuza na kununua bidhaa zao mtandaoni kupitia duka hilo.

"Tumeanzisha Duka Mtandao ninachotaka kuona ni Posta inakuwa kitovu cha biashara mtandao ndani ya nchi, na mhakikishe mnaboresha mifumo yenu ili twende kidigitali". Alisema Dkt. Ndugulile.

Sambamba na hilo, Dkt. Ndugulile ameeleza mwelekeo wa Serikali katika kulitumia Shirika la Posta katika kuwafikia wananchi kwani imetekeleza uanzishwaji wa mradi wa Huduma Pamoja(One Stop Center) ambapo mradi huo utahusisha utoaji wa huduma zote za Serikali katika ofisi za Shirika la Posta nchini.

Kwa sasa mradi huo kupitia Shirka la Posta Tanzania umekamilika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma na huduma zitakazokuwa zinapatikana ni pamoja na huduma za NIDA, TRA, RITA, Leseni za Biashara, Usajili wa Wanachama wapya wa NSSF, Usajili wa Biashara kupitia BRELA pamoja na Huduma za Uhamiaji.

Pia, Dkt. Ndugulile ametumia nafasi hiyo kutoa rai kwa Mameneja wa Mikoa ya Posta nchini kuhakikisha wanakuwa wabunifu na kutafuta fursa za kibiashara katika mikoa yao, ili kuongeza mapato ya Shirika yatakayoleta tija kwa Taifa. Pia aliwataka Viongozi hao wakawe wasimamizi wa huduma zinazotolewa katika mikoa husika ili kila mwananchi anufaike na huduma za Posta nchini.

Sambamba na hilo, Dkt. Ndugulile ameeleza kuridhishwa kwake na kasi ya utendaji ya Shirika la Posta Tanzania chini ya uongozi wa Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika hilo Bwa. Macrice Daniel Mbodo, hususani katika nyanja za mashirikiano na Taasisi nyingine kwa lengo la kukuza mahusiano, kulitangaza Shirika, kuongeza masoko na hatimaye kuongeza pato la Shirika.

Ikumbukwe kuwa hivi karibuni Shirika la Posta limeingia makubaliano ya kibiashara na Taasisi kadhaa nchini ikiweko TANTRADE, ZIC na CRDB, lengo ikiwa ni kupanua wigo wa utoaji wa huduma kwa wananchi

Naye Mkurugenzi wa Mawasiliano Serikalini Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhandisi Clarence lchwekeleza akimuwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Zainab Chaula ameendelea kulipongeza Shirika la Posta kwa namna linavyoendelea kuboresha huduma zake na kuwasisitizia uwepo wa ushirikiano kati ya viongozi hao ili kurahisiha utendaji kazi wa kila siku.

"Niwapongeze sana kwa kuwa Posta ya sasa ina vitu tofauti na bora zaidi sio kama zamani, Ila msiache kutembea pamoja katika utendaji mana kutembea pamoja kunalipa". Alisema Ichwekeleza.

Kwa upande wa Kaimu Postamata Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bwa. Macrice Mbodo amemshukuru Waziri Ndugulile kwa kutenga muda wake nakuja kufungua kikao hiki cha viongozi wa Posta nakuahidi baada ya kikao hicho Posta itabadilika na itakuwa Posta mpya, uwajibikaji utaongezeka na wafanyakazi watafanya kazi kwa kujituma na kuyatimiza malengo na maazimio yaliyowekwa na Serikali katika kuliboresha Shirika la Posta.

"Tunatarajia baada ya kikao kazi hiki, Shirika litabadilika, utendaji kazi wake utaongezeka, uwajibikaji utaongezeka na wafanyakazi watafanyakazi kwa kujituma na hakika tutatimiza ndoto na maazimio ya Serikali yetu" Alisema Mbodo.

Kikao hicho kilifanyika katika jengo la NSSF jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mameneja Wakuu wa Shirika la Posta Tanzania, Mameneja wa Makao Makuu ya Shirika, Mameneja wa Mikoa wa Posta na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi.

# NENDENI MKAYATEKELEZE MLIYOYAAZIMIA KWENYE KIKAO KAZI- MHANDISI KUNDO

Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Kundo Andrea Mathew amewataka Mameneja wa Mikoa na wale wa Makao Makuu wa Shirika la Posta Tanzania kutekeleza yale waliyoazimia kwenye kikao cha kutathmini utendaji kazi wa Viongozi wa Shirika la Posta Tanzania kwa mwaka uliopita 2020/2021 na kukubaliana malengo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mhandisi Kundo ameyasema hayo tarehe 6 Agost 2021, Jijini Dar e's Salaam, alipokuwa akifunga rasmi kikao kazi hicho cha siku tano ambacho pamoja na mambo mengine kilijadili Mpango Mkakati wa Shirika kwa mwaka 2021/2022.

"Mliyokubaliana hapa mkayatekeleze kwa pamoja kwa kuzingatia weledi na nidhamu ndani ya Shirika" alizungumza Mhandisi Kundo.

Aidha Naibu Waziri Kundo aliwataka viongozi Wakuu wa Shirika kuwawezesha vifaa vya kisasa Mameneja wa Mikoa ili wawe na wigo mpana na uhuru wa kutekeleza majukumu yao ya kazi badala ya Makao Makuu kuwa msemaji wa mwisho wa utekelezaji wa majukumu ya Shirika Mikoani.

Nae Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Ndugu Macrice Daniel Mbodo alielezea namna Viongozi hao wa Shirika walivyopata semina mbalimbali za Itifaki "Protocol", matumizi ya mifumo pamoja na uwajibikaji pamoja na utendaji wenye tija ndani ya Shirika.

Aidha Ndugu Mbodo amemshukuru Naibu Waziri Kundo kwa kuweza kufika na kufunga kikao hicho na kuahidi kuifanyia kazi mikakati waliyojiwekea pamoja na yale yaliyoagizwa na Wizara kwa maendeleo ya Shirika.




Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Kundo Andrea Mathew

# MKURUGENZI MKUU WA POSTA IVORY COAST ATEMBELEA POSTA TANZANIA




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta la Ivory Coast ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika (PAPU) na Umoja wa Posta Duniani (UPU), Ndugu Isaac Gnamba Yao ametembelea Makao Makuu ya Shirika la Posta Jijini Dar e's Salaam na kujionea namna Shirika hilo linavyofanya kazi zake hasa katika kipindi hiki cha ukuaji wa Teknolojia.

Ziara hiyo iliyofanyika tarehe 13 Septemba, ililenga kukuza ushirikiano baina ya Posta za Nchi hizi mbili pamoja na kuangalia fursa za kibiashara zitakazowezesha kukuza pato la mashirika haya.

Katika ziara yake Ndugu Isaac, alipokelewa na Meneja Mkuu Uendeshaji wa Biashara za Shirika la Posta Tanzania, Ndugu Constantine Kasese ambae alieleza hatua mbalimbali zilizofikiwa na Shirika la Posta Tanzania katika utoaji huduma kiteknolojia.

.

Aidha Ndugu Isaac alipata nafasi ya kuongea na Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania huku akiwataka kuongeza bidii na kuwa wanyumbufu katika kutoa huduma kwa niaba ya Serikali Ili kuwafikia wananchi.

Alisisitiza kuwa, Posta ni Taasisi pekee iliyo karibu na wananchi, na Serikali Inahitaji kuwafikia Wananchi wake , hivyo basi kupitia Posta, Serikali itaweza kuwafikia wananchi wengi kwa urahisi.

Katika kukamilish Ziara yake , kiongozi huyo alitembelea Posta Kuu ya Dar e's Salaam (GPO) na kujionea huduma mbalimbali zinazotolewa katika ofisi hiyo ikiwemo kituo cha "Huduma pamoja".

# HUDUMA PAMOJA



# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAPOKEA UGENI KUTOKA SHIRIKA LA POSTA BURUNDI

Shirika la Posta Tanzania ilipokea ujumbe wa viongozi waandamizi kutoka Shirika la Posta la Burundi (RNP). Ujumbe huo ulioongozwa na Mkurugenzi Mkuu Bi. Lea Ngabire akiambatana na Bwana Olivier Ndaishimiye kutoka Kitengo cha IT pamoja na Bwana Deo Misirakuba Kutoka ldara ya uendeshaji wa barua ya Shirika hilo.

Posta Burundi wamelazimika kuja Posta Tanzania wakiwa na lengo la kubadilishana uzoefu hususan kwenye eneo la uendeshaji wa huduma za Posta kidijitali ambako Shirika la Posta kwa sasa limejidhatiti.


Akizungumza wakati wa kuukaribisha ugeni huo, Kaimu Postamasta Mkuu Bwana Macrice Mbodo alisema ugeni huo ni wa faraja sana kwa Tanzania hususan Shirika la Posta Tanzania ikizingatiwa mahusiano mazuri yaliyopo baina ya nchi hizi mbili ambayo si tu kuwa ni ya kirafiki bali ni ya kidugu.

"Kama mnavyofahamu hivi karibuni Rais wa Burundi Mhe. Evariste Ndaishimiye alitembelea Tanzania na kukutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa ngazi ya kitaifa, leo na sisi Mashirika ya Posta tumefuata nyayo za viongozi wetu wakuu ndiyo maana unaona Posta ya Burundi na uongozi mzito upo hapa kwetu kwenye ziara ya kikazi na kubadilishana ujuzi". alisema Bw. Mbodo.

Kaimu Postamasta Mkuu aliongeza kuwa, maboresho ya kiutendaji pamoja na mifumo ya uendeshaji wa Shirika la Posta nchini vimekuwa chachu na kivutio kwa nchi nyingi wanachama wa Umoja wa Posta Barani Afrika (PAPU) hadi kupelekea nchi nyingi kutaka kutembelea na kujifunza kutoka Posta ya Tanzania.

Ikumbukwe kuwa, Tanzania iliweza kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania duniani kupitia Shirika la Posta Tanzania kufuatia kushinda nafasi mbili za ujumbe wa mabaraza muhimu ya Utawala na lile la Uendeshaji ya Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwenye chaguzi zilizofanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa 27 wa UPU nchini lvory Coast mwezi Agosti, 2021.

Sambamba na hilo Tanzania iliaminiwa kuongoza Kamati nyeti na muhimu ya Huduma za Posta na Biashara Mtandao (Physical Services and E-Commerce) ikiwa ni Mwenyekiti mwenza pamoja na Uswisi, nchi yenye mafanikio makubwa kwa utoaji wa huduma zenye ubora kabisa zinazoendana na teknolojia za kisasa za kiposta Duniani.



# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAPOKEA UGENI KUTOKA SHIRIKA LA POSTA BURUNDI

Bwana Mbodo aliongeza kuwa Tanzania ni mwenyeji wa Umoja wa Posta Barani Afrika, Makao Makuu yake yakiwa jijini Arusha, Kama ilivyo Uswisi ni nchi mwenyeji wa Umoja wa Posta Duniani, Makao yake Makuu yakiwa kwenye mji wa Berne na posta yao ni ya mfano Duniani, tunataka pia Posta Tanzania iwe Posta ya mfano Barani Afrika na nchi mbalimbali za Afrika zije kujifunza uendeshaji wa huduma za posta za kidijitali ndani ya Shirika la Posta Tanzania.

"Huu ndiyo mwelekeo wetu na tungependa wananchi wayajue haya na waendelee kutuunga mkono tunapotekeleza azma ya kiongozi wetu wa awamu ya sita Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye ameifungua nchi kimataifa ili kuleta uwekezaji wa kiuchumi kwa ustawi wa watanzania" aliongeza Bw. Mbodo.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu Bi. Lea Ngabire ameishukuru Serikali ya Tanzania kupitia
Shirika la Posta nchini kwa kupokea ujio wao na kukubali kubadilishana uzoefu kwa kuwafundisha mbinu na namna mbalimbali za kuendesha mifumo ya kiposta katika kutoa huduma bora kwa wananchi. Pia Bi. Lea amekiri kujifunza vya kutosha kutoka Shirika la Posta nchini na kuahidi kuutumia ujuzi huo kuboresha huduma za kiposta nchini Burundi.

Katika hatua nyingine, Bi. Lea amekabidhi zawadi kwa baadhi ya viongozi wa Shirika la Posta
Tanzania kama ishara ya kuendeleza mahusiano na mashirikiano mazuri ya Taasisi hizi mbili.



# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA LAPOKEA UGENI KUTOKA SHIRIKA LA POSTA BURUNDI






# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (kushoto) akikabidhi zawadi kwa Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo (kulia), mara baada ya kikao na Menejimenti ya Shirika la Posta pamoja na waandishi wa habari (hawapo pichani), katika Makao Makuu ya Shirika la Posta nchini, jijini Dar es Salaam.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (kushoto) akikabidhi zawadi kwa kaimu Meneja Mkuu, Uendeshaji wa Biashara za Shirika Constantine Kasese (kulia) mara baada ya kikao na Menejimenti ya Shirika la Posta pamoja na waandishi wa habari (hawapo pichani) makao makuu ya Shirika la Posta Jijini Dar es Salaam.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (kushoto) akikabidhi zawadi kwa Kaimu Meneja Mkuu Rasilimali za Shirika la Posta Aron Samwel (kulia) mara baada ya kikao na Menejimenti ya Shirika la Posta pamoja na waandishi wa habari (hawapo pichani), katika Makao Makuu ya Shirika la Posta nchini, jijini Dar es Salaam.




Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Macrice Daniel Mbodo akizungumza wakati wa kikao cha Menejimenti ya Shirika hilo na ugeni kutoka Burundi, katika Makao Makuu ya Shirika hilo, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (wa pili kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Afisa mwandamizi wa Shirika la Posta nchini Bi. Ledegunda Tarimo (kushoto) kuhusiana na namna ambavyo Shirika la Posta Tanzania linaendesha shughuli zake katika kuhudumia wananchi. Kulia ni Meneja Biashara Barua na usafirishaji Bw. Jasson Kalile




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (kushoto) akizungumza kwenye kikao na Menejimenti ya Shirika la Posta nchini, mara baada ya ziara yake kwenye ofisi za Posta Kuu Dar es Salaam.Kulia ni Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI

Picha za Matukio mbalimbali wakati Mkurugenzi wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire alipofanya Kikao na Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania, Makao makuu jijini Dar es salaam
















# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (wa tatu kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Afisa mwandamizi wa Shirika la Posta nchini Bi. Ledegunda Tarimo (wa tatu kushoto) kuhusiana na namna ambavyo Shirika la Posta Tanzania linaendesha shughuli zake katika kuhudumia wananchi. Kulia ni Meneja Biashara ya Barua na usafirishaji Jasson Kalile anayefuata wa pili kulia ni Meneja Mkoa Dar es Salamaa wa Shirika la Posta nchini Bw. Arubee Ngaruka





Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire (aliyekaa kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watendaji wa Shirika la Posta Tanzania, mara baada ya kikao chao, Makao Makuu ya Shirika hilo, jijini Dar es Salaam. Aliyekaa kulia ni Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta nchini Bw. Macrice Daniel Mbodo.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI

Picha za Matukio mbalimbali wakati Mkurugenzi wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire alipofanya Kikao na Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania, Makao makuu jijini Dar es salaam







# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI




Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainab Chaula (kushoto) akikabidhi saa maalum aliyoitoa kama zawadi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi Lea Ngabire (kulia) alipotembelewa na ugeni wa Shirika la Posta Burundi ofisini kwakwe jijini Dodoma (katikatia) ni Kaimu Postamasta Mkuu Bw. Macrice Mbodo.



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Mbodo akizungumza wakati wa mkutano huo.




Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainabu Chaula (kushoto) akikabidhi saa maalim aliyoitoa kama zawadi kwa Bw. Oliever Ndaishimye (wa pili) kutoka Kitengo cha IT cha Shirika la Posta Burundi.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire akizungumza wakati wa mkutano huo.



Viongozi waandamizi kutoka Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Posta Burundi wakifuatilia mkutano huo.



Mkurugenzi wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire akiwa ofisini kwa katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasilianno na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainab Chaula kabla ya kuanza kwa mkutano wao, jijini Dodoma.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI



Mkurugenzi wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasilia katika ofisi za Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), jijini Dodoma. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa UCSAF Bi. Justina Mashiba na wa tatu kushoto ni Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta nchini Bw. Macrice mbodo



Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta nchini Bw. Macrice mbodo (Kushoto) akizungumza na Mkurugenzi wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire ( Katikati) baada ya kuwasili katika ofisi za Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), jijini Dodoma. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa UCSAF Bi. Justina Mashiba.

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt. Jabir Kuwe Bakari (kulia) akifanya mazungumzo na ugeni kutoka Shirika la Posta Burundi. Wa tatu kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi. Lea Ngabire.

Posta
Let's Go!

# PICHA NA MATUKIO MBALIMBALI

Picha za Matukio mbalimbali Katika Makumbusho ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufuatia ugeni wa Shirika la Posta Burundi uliongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Posta Burundi Bi.Lea Ngabire (Kushoto, Picha ya Kwanza)






# KATIBU MKUU WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI AKUTANA NA UONGOZI KUTOKA POSTA BURUNDI



Katibu Mkuu Wizara ya habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainab Chaula amepokea ujumbe kutoka Shirika la Posta Burundi ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo Bi. Lea Ngabire kwenye Ofisi za Wizara hiyo Jijini Dodoma.

Ziara hiyo yenye lengo la kujifunza masuala mbalimbali y mawasiliano ya Posta imechagizwa na hatua iliyofikiwa na Shirika la Posta Tanzania ya kufanya mageuzi na maboresho makubwa ya mifumo ya uendeshaji wa Shirika la Posta nchini hasa katika eneo la Biashara mtandao ambapo Duka Mtandao la Posta limekuwa kivutio kwa nchi nyingi wanachama wa umoja wa Posta Africa (PAPU) na kupelekea nchi nyingi kuonyeshaa nia ya kuja kujifunza kutoka Posta ya Tanzania.

Aidha, Bi. Lea Ngabire akiwa Mkoani Dodoma akiambatana na mwenyeji wake ambae ni na Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania walimtembelea Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) Bi. Justina Mashiba kwa lengo la kuendelea kujifunza zaidi huduma za Mawasiliano kwa wote zinavyowafikia wananchi wa maenneo ya vijijini.

Hata hivyo Bi. Lea Ngabire alionyesha kufurahishwa sana na maeneo yote aliyopita kujifunza na kuahidi kuyafanyia kazi pindi arejeapo nchini kwao.

Posta
Let's Go!

# DKT. CHAULA APOKEA UGENI KUTOKA SHIRIKA LA POSTA KENYA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainab Chaula amepongeza Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Posta Kenya kwa kuendelea kuimarisha mahusiano yenye tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Hayo ameyasema wakati alipopokea ujumbe kutoka Shirika la Posta Kenya ulioongozwa na Postamasta Mkuu wa Shirika hilo Bw. Dan Kagwe aliyeambatana na Milka Mugwe, Meneja Uendeshaji na Huduma kwa Wateja pamoja na Joel Mageto,Meneja wa Miradi Maalum na Katibu katika Ofisi ya Postamasta Mkuu wa Shirika hilo, katika Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) jijini Dar es Salaam.

Dkt Chaula ameeleza kuwa kuwepo kwa mahusiano mazuri na ushirikiano wa moja kwa moja kati ya Shirika la Posta Tanzania na Shirika la Posta Kenya ni chachu ya kuendelea kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Katika hatua nyingine Dkt Chaula ameeleza kuwa ni vizuri kuboresha matumizi ya Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano na kulinda utaifa na heshima ya nchi zetu.

"Ushirikiano huu uende kuboresha utoaji huduma na biashara kati ya Kenya na Tanzania na Mashirika haya yatumike kama kitivo cha biashara na zilete fursa kwa wafanyabiashara wa pande zote mbili". amesema Dkt. Chaula.

Dkt. Chaula ameongeza kuwa Mashirika ya Posta yafungue milango ya biashara kwa wananchi ili kuleta wepesi wa upatikanaji wa huduma kwa wananchi sambamba na mahitaji yao.

Aidha, alitaka Shirika la Posta nchini kwa kushirikiana na Posta zingine Afrika kulinda tamaduni zetu kwa kuendelea kuipa kipaumbele lugha ya Kiswahili kwa lengo la kukuza na kutumika kama fursa kwa wafanyabiashara ili kuleta tija kwa Taifa.

Naye, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi alisema ni vema kujifunza kwa kushirikiana na wanapotoka nje ya Afrika Mashariki kuwa wamoja ili kuleta manufaa ya kuwa pamoja.

Ameongeza kuwa, zinapotokea fursa wanapaswa kwenda kama Washirika kutoka Afrika Mashariki na kuendelea kusisitiza taasisi hizi kuona umuhimu wa kuendelea kufanya tafiti ili kuleta maendeleo kwani tafiti zitawasaidia kuongeza maarifa, uelewa na kuongeza ubunifu katika kuhudumia wananchi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt. Jabiri Bakari alimshukuru Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Kenya Bw. Dan Kagwe kwa kuja kutembelea Tanzania na kujionea maboresho yanayoendelea kufanywa na Shirika la Posta Tanzania.



# DKT. CHAULA APOKEA UGENI KUTOKA SHIRIKA LA POSTA KENYA


Naye, Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Bw. Macrice Daniel Mbodo, aliielezea mikakati ambayo Shirika la Posta nchini linayo ili kukuza mahusiano kati yake na Posta zingine Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla, urahisisha utoaji wa huduma za kiposta Barani Afrika.

Bw. Mbodo amesema kuwa kwa sasa Posta ni zaidi ya barua, Shirika linaendelea kuboresha huduma zake na kuzitanua zaidi ili kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuwa Posta Tanzania inaenda kuwa ya mfano Bara la Afrika.

Kaimu Postamasta Mkuu ameongeza kuwa kutokana na maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika ndani ya Shirika la Posta nchini, wanatarajia kupokea ugeni kutoka nchi mbalimbalimba za Afrika ikiwemo Congo Brazzaville, Zimbabwe, Oman na nchi zingine za Afrika.

Kwa upande wake, Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Kenya Bw. Dan Kagwe ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa mapokezi makubwa na ushirikiano mkubwa aliopata katika ziara yake ya kujifunza na kubadilishana uzoefu.





Vilevile, Bw. Kagwe ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuboresha na kuimarisha Sekta ya Posta nchini ili kuhakikisha linatoa huduma stahiki kwa wananchi na kwa kutumia mifumo ya kidijitali inayofanya wananchi wengi wanahudumiwa kwa wakati

Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Kenya Bw. Kagwe ametoa mwaliko kwa Viongozi wa Shirika na Wizara kutembelea Kenya ili kuendelea kujenga mahusiano na kubadilishana uzoefu ili kuhudumia jamii zetu.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainab Chaula alikabidhi zawadi kwa Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Kenya Bw. Dan Kagwe pamoja na maafisa waandamizi walioongozana naye.

Posta
Let's Go!

# WADAU WETU

Wizara ya habari
Mawasiliano na
Teknolojia ya habari

# HUDUMA ZETU

Posta
Let's Go!

# TANZANIA POSTS CORPORATION


HEAD OFFICE: POSTA HOUSE 12th FLOOR,7 GHANA STREET,

P.O.Box 9551, 11300 Dar es Salaam, Tanzania

Fax: (022) 2113081 Mobile: (022)2113394/2111715/2118280

Phone: +255 738 070 702

Email: pmg@posta.co.tz

Website: www.posta.co.tz


posta_tz